
PURPOSEFUL PARENTING
ACADEMY
MALEZI 1001
Yaliyo Muhimu

# MALEZI 101

## Muhtasari wa Mambo Muhimu

PURPOSEFUL PARENTING
ACADEMY

**Dr. Gladness Temu**



2

# 1. MALEZI YANAHUSU WEWE MZAZI

Malezi ni kuhusu wewe mzazi, si kuhusu mtoto!

Ni wewe ambaye unakwenda kumlea mtoto!

Ni wewe unayehitaji maarifa, ujuzi na uelewa!

Ni wewe ambaye unatakiwa uwe mzazi (kuwa katika kitendo cha kulea)!

Ni wewe ambaye Mungu amekukabidhi jukumu la kumlea mtoto huyo!

Mtoto hajui jinsi ya kujilea mwenyewe. Kile unachojua na kile unachokuwa (au namna ulivyo) ndicho mtoto wako atakachokuwa. Unakuwa nani? Mzazi mwenye maarifa, ujuzi, na mwenye nia maalum ya kumlea mtoto ili afikie hatma Mungu aliyoikusudia au mzazi wa mawazo ya kizamani kama vile kuamini kuwa kulea ni jambo jepesi tu na la asili (natural process) na wala halihitaji kujifunza?

PURPOSEFUL PARENTING
ACADEMY

Jinsi ulivyolelewa ina umuhimu mkubwa sana maana inategemea sana ni nani alikulea, mzazi huyo alijua nini kuhusu malezi, ni katika mazingira gani ulilelewa na ni nini ulichokiona au kukumbana nacho katika safari yako ya kulelewa. Ikiwa ulilelewa na mzazi 'mjinga' ambaye hakujua athari ya kile alichokuwa akifanya kwa mtoto, basi huenda ukawa mwathirika wa tabia mbalimbali zinazotokana na malezi. Kwa mfano, ikiwa ulilelewa kwa vurugu nyingi, makelele makali (kufoka) na kupuuzwa kihisia, uwezekano wa wewe kuteseka kutokana na hayo ni mkubwa. Mzazi anayepiga kelele huzalisha mtoto anayefoka na hatimaye mtu mzima anayeongea kwa kufoka.

Watu wengi hufikiri kwamba kulea mtoto hakuhitaji mafunzo au ujuzi wowote hivyo wazazi wengi wanalea kwa majaribio. Ukilea kwa kujaribu jaribu tu hiki



3

na kile, matokeo yake ni kuwa mtoto atakuwa chochote (kwa upande wa tabia au sifa za ndani) kwa sababu alilelewa vyovyote vile. Katika Purposeful Parenting Academy (PPA) tunakataa kulea mtoto vyovyote vile. Kwa nini? Kwa sababu kuna maarifa mengi, ujuzi, na miundo mbalimbali ya malezi na mifumo inayoweza kuwawezesha wazazi kuwalea watoto wao kwa nia au malengo maalum na kwa ufanisi.

Hebu tuone baadhi ya hadithi za uongo (*myths*) kuhusu malezi ambazo zimewagharimu wazazi wengi wa leo na kuathiri vizazi vyetu.

## 2. BAADHI YA HADITHI ZA UONGO (MYTHS) KUHUSU MALEZI

### 1. Wazazi wetu hawakujifunza popote kuhusu malezi lakini walitulea vizuri.

Hii si kweli kwa sababu wao pia walijifunza malezi kutoka kwa wazee wao. Hata hivyo, wakati wao kulikuwa na maarifa machache na nafasi ndogo ya kushirikishana nje ya familia, ukoo au kijiji chao. Hali ni tofauti leo kwani kuna ongezeko kubwa la maarifa na ulimwengu umekuwa mmoja ambapo mtu yeyote anaweza kufikisha na kushirikisha maarifa hata nje ya mipaka ya kimataifa. Pili, licha ya juhudi zao za kutulea, walikosea katika maeneo mengine ambapo karibu kila mtu mzima ana maeneo mengi ya kurekebisha. Kwa mfano, baadhi ya watu wazima hukosa ujasiri, huruma, stadi za mawasiliano, udhibiti wa hisia na mengine mengi yanayohitaji maendeleo binafsi (*personal development*).

### 2. Malezi hayana mtaala (curriculum).

Hii si kweli. Malezi hutumia 'mtaala' fulani ama kwa nia maalum au bila nia maalum (intentionally or unintentionally). Jinsi unavyomlea mtoto wako ni mtaala tayari. Hata hivyo, unaweza kuamua kutumia mtaala wa kudhamiria au kumlea mtoto wako kwa kutumia mtaala wa 'vyovyote vile'. Sulemani, mfalme mwenye hekima zaidi kuwahi kuishi dunaini, aliwashauri wazazi

akisema: "Mlee mtoto katika njia impasayo; Naye hataiacha hata atakapokuwa mzee." Basi, kuna 'njia impasayo mtoto kuifuata'! Kwa maneno mengine, kuna 'ramani ya maisha' ya jinsi mtoto anavyotakiwa kwenda. Hii yenyewe tu ni mtaala!

3. **Hakuna ubobezi (expertism) katika malezi. Ikiwa ni mtoto wa kuwa na tabia njema atakuwa na tabia. Ikiwa ni mtoto wa kuharibika ataharibika tu**

Huu ni uwongo unaotoka kuzimu! Mungu hawezi kumfanyia binadamu hili. Kumleta mtoto duniani na kisha kumwacha apotee kutokana na matatizo ya tabia si mpango wake. Hakuna mtu aliyezaliwa ili apotee. Malezi ni uwanja/safari iliyojaa maarifa, ujuzi, miundo, mikakati, ratiba, mifumo na mengine mengi; na haya yote yanapatikana. Hakuna jambo linaloweza kufanywa vizuri bila kujifunza, vivyo hivyo unahitaji kujifunza malezi ili uweze kulea vyema/ipasavyo.

4. **Mtu yeyote anaweza kumlea mtoto kwa jinsi yoyote anavyotaka**

PURPOSEFUL PARENTING ACADEMY

Hii ni *myth* nyingine kubwa ya uongo ambayo haina mashiko. Kila mtoto (au tuseme kila mtu) alikuja duniani kwa kusudi. Na kwa sababu ya kuwa na makusudi tofauti tofauti, kila mtoto (mtu) ni wa kipekee. Na kutokana na upekee wa kila mtu, kila mtoto ana ramani ya maisha ya kipekee. Kwa hivyo, huwezi kumlea mtoto jinsi unavyotaka, vinginevyo utaharibu kusudi lake (hatma yake). Isitoshe, mtoto si wako (wazazi). Mtoto huja kutoka kwa Mungu kama baraka kwa ulimwengu kupitia wazazi. Hata Serikali ina mamlaka juu ya mtoto wako! Huwezi kumfanyia jambo lolote (lililokatazwa na sheria za Serikali) mtoto wako eti kwa sababu mtoto 'ni wako'! Hivyo huwezi tu kuamua kumlea unavyojiskia au unavyopenda wewe, utamharibu, utaharibu hatma yake.



5

5. **Mtoto atakua tu hata kama wazazi hawatajifunza au kutumia stadi za malezi.**

Hii ni KWELI. Mtoto atakua tu hata bila kulelewa kwani wakati kukua ni mchakato wa asili, malezi si hivyo. Kwa hivyo, ingawa mtoto wako atakua, lakini atakua mtu mzima wa aina gani? Wazazi wenye maarifa na ujuzi wana nafasi nzuri zaidi ya kulea watu wazima walio na tabia na mwenendo unaofaa kwao binafsi na kwa jamii. Kwa hivyo, malezi na matunzo ni tofauti ingawa kumtunza mtoto ni sehemu muhimu ya malezi. Hata hivyo, kumpa mtoto vitu kama chakula, nguo, malazi, na elimu rasmi ya shule hakujumuishi maana kamili na halisi ya malezi. Malezi ni kumfundisha mtoto (kumrekebisha, kumwongoza, kumfunza, kumshauri, kumelimisha, kumboresha, kumuandaa, kumuonya,kumtengeneza, kumuadibisha, kumuweka tayari kwa ulimwengu wake, kumkochi nk kumpa mazoezi n.k.).

6. **Malezi ni kuhusu mtoto zaidi.**

Hapana. Malezi ni kuhusu wewe mzazi kwanza, kama ilivyoelezwa hapo juu. Mtoto hajilei mwenyewe.

PURPOSEFUL PARENTING ACADEMY

7. **Unaweza kumlea mtoto wako vizuri, lakini marafiki/ulimwengu wanaweza kumbadilisha mtoto.**

Ndio na Hapana. Kile kinachodhaniwa kuwa ni 'malezi mazuri' huenda yasiwe mazuri kwa maana halisi. Ili kuwa malezi mazuri kuna vigezo. Mfano jiulize wewe kama mzazi unaleaje? Unajua nini (una maarifa kiasi gani) kuhusu malezi? Ni mifumo gani umeiweka katika mazingira yako ya nyumbani? Je, mna ratiba, miundo na zana mnazofuata au mnayotumia katika malezi yenu? Je, unakua na kukomaa pia kama mzazi? (unaongezeka katika hekima, maarifa na uelewa katika masuala mazima ya malezi?).



6

Ikiwa mtoto amelelewa vizuri kwa kutumia miundo, mifumo na mikakati inayofaa ya familia na malezi, kuna uwezekano mkubwa kwamba tunu (*values*) zilizowekezwa ndani yake zitakuwa sehemu muhimu ya mtoto huyo hadi uzeeni. Hivyo basi mazingira/ulimwengu huenda yakambadilisha mtoto wako au yasimbadilishe kulingana na mfumo uliotumia kumlea. Mtoto wako anaweza kuubadilisha ulimwengu (marafiki zake wa rika moja) kuelekea kwake na si lazima yeye avutwe na ulimwengu au marafiki wabaya.

8. **Hata nisipojifunza malezi watoto wangu bado watakua na kuwa watu wazima wazuri**

Ni kweli na pia si kweli. Usipojifunza malezi bado kuna elimu au maarifa fulani utakayokuwa unayatumia kwa kujua au bila kujua. Hiyo elimu au hayo maarifa yanaweza kuwa ni bora au yakawa yana upotoshaji na hivyo kusababisha athari chanya au hasi kwa mtoto wako. Hata hivyo, sula la mtoto kukua atakua tu na kufikia utu uzima sababu kukua (na kuongezeka umri) ni suala la kiasili., ila atakuwa mtu mzima wa namna gani, hilo hatuwezi kuwa na majibu kwa sasa ila inawezekana akawa mtu mzima  mwenye 'viraka vingi' kwenye tabia.

PURPOSEFUL PARENTING
ACADEMY



7

Kwa maswali au mawasiliano zaidi tembelea kurasa zetu:

Instagram: purposeful_parentingacademy | dr_gladyparenting

Email: info@ppa.co.tz  Simu: +255759207620

Tovuti:  www.ppa.co.tz

©Purposeful Parenting Academy 2025

PURPOSEFUL PARENTING
ACADEMY



8